**Wespath Benefits and Investments**
1901 Chestnut Avenue
Glenview, IL 60025-1604
wespath.org

**Wamethodisti Wawili Mashuhuri Watasadia Kuongoza Mazungumzo ya Usimamizi Mwaminifu**

Wespath inafuraha kutangaza kwamba Mchungaji Laura B. Kigweba na Mchungaji Neal Christie wamejiunga na Wespath na wataunga mkono juhudi za shirika hilo za kuishirikisha Kanisa La Muungano la Methodisti duniani kote (UMC) katika mazungumzo kuhusu usimamizi mwaminifu wa fedha na rasilimali.

Mchungaji Kigweba ni shemasi wa muda katika Mkutano wa Baltimore-Washington na amehudumu katika Kanisa la UMC kwa zaidi ya miaka 10. Amehudumu kama mkurugenzi wa zamani wa Jumuiya kwa Baraza Kuu la Kanisa na Jamii la UMC (General Board of Church and Society). Katika jukumu hilo alifanya kazi kwa kina na viongozi katika Eneo la Episkopali la Zimbabwe, Kenya na Ufilipino (Philippines), akijikita katika haki ya hali ya hewa na mazingira. Mchungaji Kigweba alijiunga na Wespath mwezi Januari kama Mkurugenzi wa Usimamizi wa Uwekezaji Endelevu na Uhusiano na Kanisa.

Mchungaji Christie ni shemasi aliyeteuliwa mwenye uanachama kamili katika Mkutano Mkuu wa Greater New Jersey na mjumbe mshiriki wa Mkutano wa Baltimore-Washington na amehudumu katika Kanisa la UMC kwa zaidi ya miaka 35. Amefanya kazi katika makanisa ya mitaa na kama mfanyakazi wa mkutano. Aidha, Mchungaji Christie pia alihudumu kama afisa mkuu wa zamani katika Idara ya Kanisa na Jamii (Church and Society). Alikuwa msimamizi mkuu wa mchakato wa ushiriki wa UMC kuhusu Kanuni za Kijamii Zilizorekebishwa. Mchungaji Christie atahudumu kama mshauri wa Wespath.

Wespath ilimwajiri Mchungaji Kigweba na kumshirikisha Mchungaji Christie ili kuongeza uwezo wa shirika la kujibu maoni yaliyopokelewa mwaka jana. Mnamo Septemba 2025, Wespath iliandaa mkutano ulioangazia Kifungu cha 717, sehemu katika *Kitabu cha Nidhamu* (*The Book of Discipline*) inayoelezea jinsi Wespath na vyombo vingine vya UMC lazima vijitoe kudumisha maadili ya UMC. Mkutano huo uliandaliwa kama mwanzo wa mazungumzo ya kiunganishi kuhusu kurekebisha Kifungu cha 717 katika Mkutano Mkuu wa 2028. Majadiliano na wahudhuriaji yaliweka mambo mawili wazi: Kanuni za Kijamii (Social Principles) zinapaswa kubaki kuwa kigezo kikuu na Wespath inahitaji kualika sauti zaidi kutoka nje ya Marekani katika mjadala huo.

Maoni haya yaliihimiza Wespath kutafakari jinsi ya kujumuisha mapendekezo haya na pia kutathmini upya wigo wa kazi hiyo. Pamoja na kuendeleza mchakato wa ushirikiano unaolenga kuandaa sheria ya Kifungu cha 717 inayoungwa mkono na wengi, sasa Wespath pia inatafuta kuwa na mazungumzo na Kanisa la UMC duniani kote kuhusu maana ya kuwa msimamizi mwaminifu wa pesa na rasilimali kwa mujibu wa Kanuni za Kijamii (Social Principles).

Mchungaji Kigweba na Mchungaji Christie wanaleta utaalamu wa kina kuhusu Kanuni za Kijamii (Social Principles) katika mchakato wa Wespath. Zaidi ya hayo, ingawa Wespath ina uzoefu wa kushirikiana na UMC duniani kote kuhusu mada zinazohusiana na uwekezaji na manufaa, kuongezwa kwa Mchungaji Kigweba na Mchungaji Christie kutasaidia Wespath kuwezesha mawasiliano na mazungumzo imara zaidi na WaMethodisti wa Muungano barani Afrika, Ufilipino na Ulaya.

"Ninajisikia mwenye bahati sana kuwa na Laura na Neal katika timu yetu," alisema Jake Barnett, Mkurugenzi Mkuu wa Mikakati ya Uwekezaji Endelevu  wa Wespath. "Wanaleta uzoefu mkubwa katika

majukumu yao na watatusaidia kusikia mitazamo, matarajio na mahitaji ya Wametodisti wa Muungano katika Marekani na nje ya Marekani.

"Mawasiliano yao kote duniani yatakuwa na manufaa makubwa, lakini nadhani mawazo yao, kanuni na tabia yao ya ujumuishi vitakuwa na athari kubwa zaidi kwenye kile tutakachofanikisha pamoja."

Ikiwa ungependa kufuatilia juhudi za Wespath zinazoendelea za kuishirikisha UMC kuhusu kuwa msimamizi mwaminifu nchini Marekani na katika makungano ya kikanda nje ya Marekani, unaweza kujisajili kupokea barua pepe zinazolenga juhudi hizo **hapa**.

***Kuhusu Wespath Benefits and Investments***

*Wespath ni shirika lisilo la faida ambalo limekuwa likihudumia Kanisa La Muungano la Methodisti (UMC) kwa zaidi ya karne moja. Kulingana na majukumu yake ya udhamini, Wespath husimamia mipango ya manufaa na, pamoja na kampuni zake tanzu, ikiwemo Wespath Institutional Investments, huwekeza karibu dola bilioni 28 katika mali kwa niaba ya washiriki zaidi ya 100,000 na taasisi zaidi ya 150 za Kikristo wa Methodisti (kufikia Desemba 31, 2025). Wespath huwekeza kwa njia endelevu inayolenga kuleta athari chanya za kifedha, kijamii na kimazingira huku ikizingatia maadili ya UMC. Wespath ina moja ya mifuko mikubwa zaidi ya pensheni inayotegemea imani duniani. Kwa maelezo zaidi kuhusu Wespath, tafadhali tufuate kwenye* ***Facebook****,* ***Instagram****,* ***LinkedIn*** *na* ***YouTube****.*